Maswali na majibu kuhusu kufunguliwa tena kwa shule za chekechea

Kwa kawaida, watoto wengi hufurahia kila mara shule za chekechea zinapofunguliwa na pia wanapoonana na marafiki zao tena. Hata hivyo, sio wazazi wote na wafanyakazi wa shule ya chekechea ambao huwa na ujasiri wa kuendelea.

Shule za chekechea zilizoko Trondheim zitafunguliwa tena Jumatatu, tarehe 20 Aprili. Manispaa ya Trondheim iliwaalika wazazi na walezi ili wawasilishe maswali yoyote ambayo wanaweza kuwa nayo. Tulipokea maswali mengi na siku ya Ijumaa, maswali haya mengi yalijibiwa wakati wa matangazo ya moja kwa moja kwenye Kituo cha Televisheni cha manispaa hiyo.

Unaweza kutazama matangazo hayo hapa:
https://trondheim.kommunetv.no/archive/481

Jopo lililojibu maswali lilihusisha Camilla Trud Nereid, mkurugenzi wa manispaa anayesimamia malezi na elimu, Ella Ingdal, meneja wa shule za chekechea katika manispaa, Betty Johanne Pettersen, afisa mkuu wa matibabu, manispaa ya Trondheim, pamoja na Gunn Kristin Hansvold, Meneja wa Shule ya Chekechea ya Øya.

Tutashirikisha baadhi ya maswali muhimu zaidi katika hati hii. Hati hii pia itatafsiriwa kwa lugha za Kiingereza, Kipolishi, Kisomali, Kifarsi, Kitigrinya, Kiarabu, Kifaransa, Kihispania na Kiswahili. Maandishi yaliyotafsiriwa yatapatikana siku ya Ijumaa.

– Ni kwa nini mnaamini kuwa ni salama kwa watoto wetu kuanza kuhudhuria shule za chekechea?
Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Pettersen: Nchini Norway na duniani kote ni watoto wachache wamepatikana na maambukizi ikilinganishwa na watu wazima. Kwa mfano, nchini Iceland na Singapore kulikuwa na watoto wachache sana kati ya wale waliopimwa. Hii inaonyesha kuwa watoto hawaambukizwi kwa haraka na hawaenezi ugonjwa huo kama watu wazima. Mara nyingi wao hawaonyeshi dalili kali na hawathiriwi sana na ugonjwa huo. Kwa sababu hii, pia tunadhania kuwa hali yao ya uambukizaji iko chini. Ni muhimu kujua kuwa katika nchi ambazo shule hazikufungwa, kumekuwa na visa vichache sana vya maambukizi kati ya watoto, na vivyo hivyo ndivyo hali ilivyo nchini Norway na Trondheim, ambapo tumekuwa na watoto katika shule za chekechea na zile za jumla.

– Je, ikiwa mzazi au mlezi ana ugonjwa wa kisukari au pumu, mtoto anapaswa kuwekwa nyumbani?

Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Pettersen: Ikiwa ugonjwa wa kisukari au pumu unaomwathiri mzazi au mlezi umedhibitiwa vyema bila matatizo, mtoto hahitaji kuwekwa nyumbani. Ushauri wa jumla wa kuzuia maambukizi na kudumisha usafi mzuri unapaswa kufuatwa katika shule ya chekechea na pia nyumbani. Ikiwa mzazi au mlezi ana umri zaidi ya 50, na ana ugonjwa ambao haujadhibitiwa vyema au ana matatizo yanayohusiana na ugonjwa huo au magonjwa mengine, mzazi au mlezi huyo anapaswa kuwasiliana na daktari wake ili kutathmini ikiwa kuna hitaji la mabadiliko kabla ya kukubalisha mtoto kurudi shuleni. Tunawaomba watu wawasiliane na shule zao za chekechea kuhusu hili.

– Je, ikiwa kuna magonjwa ya mapafu kwenye familia, kwa watoto au watu wazima, mtoto anapaswa kuwekwa nyumbani?

Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Pettersen: Magonjwa ya mapafu ni kati ya magonjwa ambayo *yanaweza kuongeza* hatari kubwa mwilini kwa sababu ya COVID-19, haswa iwapo kazi ya mapafu imepunguzwa kwa kiasi kikubwa. Hatua za kuzuia maambukizi lazima zichukuliwe nyumbani, na shule za chekechea zitajitahidi sana katika suala hili. Wazazi na walezi walio na ugonjwa wa mapafu wanapaswa kuwasiliana na daktari wao ili kutathmini hitaji la mabadiliko yanayohusiana na mtoto kurudi shuleni ili kupunguza hatari ya kuambukizwa nyumbani. Iwapo watoto wana wazazi au walezi (au wengine nyumbani) walio katika kikundi kilicho hatarini, mazungumzo yanapaswa kuanzishwa kati ya shule ya chekechea na wazazi au walezi hao kuhusu uwezekano wa kukabiliana na hali hiyo.

– Je, tofauti kati ya dalili za maambukizi yanayohusiana na kupumua na homa ya kawaida ya mapua iko wapi? Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Pettersen: Watoto wengi mara nyingi huwa na homa ya kawaida ya mapua bila dalili zingine za maambukizi yanayohusiana na kupumua, haswa ikiwa wamekuwa nje ya nyumba. Watoto hawa wanaweza kuhudhuria shule ya chekechea mradi tu wawe na afya njema. Ikiwa dalili za mtoto zinabadilika na anaonekana amechoka zaidi, ni mgonjwa na ana homa, maambukizi yanahusiana na kupumua yatashukiwa.

– Je, ni hatua gani za kuzuia maambukizi ambazo mnatarajia zifuatwe katika shule za chekechea?

Meneja Gunn Kristin Hansvold: Wafanyakazi wote wamekamilisha mafundisho kamili kuhusu uzuiaji wa maambukizi. Maelezo thabiti pamoja na ukuzaji wa uzoefu ni muhimu katika usalama wa wafanyakazi. Jana, tulipokea mwongozo mzuri wa kuzuia maambukizi. Haswa, kuna mambo matatu ambayo tunapaswa kuzingatia: Mambo ya kufanya kwa kiwango cha chini watoto na watu wazima wanapokuwa na dalili. Usafi mzuri, ambao sisi huzingatia kila mara katika shule ya chekechea na ambao tumezidisha. Na usafishaji bora. Ni lazima wafanyakazi wote watarajie kufanya baadhi ya majukumu ya kusafisha. Lazima tujizuie kukaribiana na wengine na tujipange katika vikundi vidogo vilivyo na wafanyakazi wasiobadilika mara kwa mara. Watoto wanapaswa kuruhusiwa kucheza katika vikundi vilivyowekwa.

– Je, kutakuwa na mpangilio wa saa za kuwaleta na kuwachukua watoto ili kupunguza hali ya kutangamana kwa karibu?

Meneja Gunn Kristin Hansvold: Kwa sasa tunatathmini mahitaji ya wazazi kuhusu saa zetu za kufungua. Tutakuwa na mtazamo wa saa ambazo wengi wanafika na kisha tutachukua hatua kadhaa katika suala hili. Tutakuwa na ushirikiano mzuri na kikundi cha wazazi, ili hili

liweze kutekelezwa kwa njia bora zaidi.

– Mnakusudiaje kupunguza hatari ya kuambukizwa kwa watoto wadogo, ambao mara nyingi hula na kuonja vipengee vya vyakula kwa pamoja, na hawaelewi kuwa hawahitaji kukaribiana?
Meneja Gunn Kristin Hansvold: Kupitia kupanga mazingira ya ndani na kwa kutoa maoni mazuri kuhusu vifaa vya kuchezea ambavyo vitapatikana. Vifaa vichache vya kuchezea vitapatikana, na tunahitaji kuwa na mtazamo mzuri na kudhibiti hali hii. Pia, tutafuatilia kwa karibu mambo ya usafi.

– Saa za kufunguliwa kwa shule za chekechea zitapunguzwa?
Meneja Gunn Kristin Hansvold: Hii inaweza kuwa chaguo kwa wengine lakini, tena, tunategemea tathmini ya mahitaji ya wazazi.

– Je, una rasilimali / wafanyakazi wa kutosha unapogawa vikundi vidogo, na wakati wafanyakazi wengine hawawezi kufanya kazi ikiwa wako katika kikundi kilicho katika hatari na / au ambao wana dalili?
Meneja wa Manispaa Ella Ingdal: Ukubwa wa kikundi unaorejelewa katika mwongozo unalingana na mahitaji ya chini katika uajiri wa wafanyakazi wa shule za chekechea. Kwa utekelezaji, hili linarahisisha uundaji wa vikundi. Ikiwa baadhi ya wafanyakazi wa shule ya chekechea watokosekana kazini kwa muda tajika, itatubidi kuzingatia kuwaajiri wafanyakazi wengine kwa muda mfupi. Hii ni hatua ya kawaida katika shule za chekechea iwapo wafanyakazi watakosa kuja kazini.

– Ninaweza kuwa na uhakika kuwa mtoto wangu hatakutana na watu wazima wapya kila siku na kuwa ataendelea kuonekana?
Meneja wa Manispaa Ella Ingdal: Wanaweza kuwa na uhakika kwa hilo.

– Kuna kitu chochote wazazi wanapaswa kumtuma mtoto nacho, au kutomtuma nacho anapoenda shule ya chekechea?
Meneja Gunn Kristin Hansvold: Hatutaki vifaa vya kuchezea kutoka nyumbani. Midoli pamoja na vifaa vya kuwekwa kwenye vinywa ya watoto bila shaka zinakubalika. Mavazi bado yanaweza kuachwa katika eneo la kubadilishia nguo. Tunahitaji muda kuandaa maelezo thabiti yatakayotumiwa na vikundi vyetu vya wazazi. Ushirikiano mzuri wa wazazi na walezi utakuwa muhimu.

– Je, watoto wanaweza kucheza pamoja, na pia kucheza na yeyote watakao?
Meneja Gunn Kristin Hansvold: Ndiyo, na wale ambao ni wa kikundi chao.

– Sehemu na vifaa vya kuchezea zinasafishwa vipi na mara ngapi?
Meneja Gunn Kristin Hansvold: Tutasafisha mara nyingi zaidi kuliko hapo awali. Vyoo na maeneo ya kunawia mikono zitasafishwa angalau mara moja kwa siku. Isitoshe, sehemu za maeneo zitasafishwa mara mbili hadi tatu kwa siku. Ratiba yetu ya kusafisha itaimarishwa.

- Kuna miongozo yoyote iliyowekwa kuhusu wafanyakazi wa muda mfupi? Je, wafanyakazi wengi wa muda mfupi wanafanya kazi katika shule za chekechea na

shule zinginezo? Na je, wako huru kufanya kazi katika shule hizi zote, uwezekano wa maambukizi ukizingatiwa?
Meneja wa Manispaa Ella Ingdal: Wafanyakazi wote watamaliza mafunzo kuhusu uzuiaji wa maambukizi. Hii pia inatumika kwa wafanyakazi wa muda mfupi. Usimamizi wa shule za chekechea una jukumu katika utekelezaji wa jambo hili. Jinsi mambo yalivyo, hatupendekezi kwamba wafanyakazi wa muda mfupi wahame baina ya shule kadha wa kadha za chekechea.

- Ikiwa itashauriwa kwamba mtoto wangu awekwe nyumbani, bado itanilazimu kulipia mahali pa chekechea?
Mkurugenzi wa manispaa Camilla Trud Nereid: Ikiwa mtoto anaweza kuhudhuria shule ya chekechea, basi mtoto anapaswa kuwa akihudhuria shule ya chekechea na kwa hivyo mzazi pia atalazimika kulipia mahali pa chekechea. Ikiwa itashauriwa kwamba mtoto awekwe nyumbani, tutazingatia hili kwa hali ya mtu binafsi.

- Je, Manispaa inapendelea kwamba sisi ambao tuna uwezo wa kuwaweka watoto wetu nyumbani, tufanye hivyo ili kupunguza idadi ya watoto katika shule za chekechea, na kwa hivyo kupunguza hatari ya kuambukizwa?
Mkurugenzi wa manispaa Camilla Trud Nereid: Ikizingatiwa kwamba watoto hawana hatari kubwa ya kuambukizwa, na tunapozingatia manufaa ambayo shule za chekechea zinatoa kwa watoto wanaohudhuria, tunapendekeza kwamba wale ambao wanaweza kwa sasa wahudhurie shule hizo.

- Nina wasiwasi kuhusiana na kufunguliwa tena kwa shule za chekechea. Nimesoma baadhi ya matokeo ya utafiti wa kisayansi ambao umefanywa kuhusu COVID-19. Tafiti kadhaa kutoka nje ya nchi zinaonyesha kuwa watoto wanaweza kuambukizwa kwa hakika, lakini mara nyingi huwa hawana dalili za maambukizi. Mazingira yenye watoto yanaonyesha hatari kubwa ya usambazaji wa maambukizi, kama ilivyoonekana kwenye Shule ya Flatåsen msimu uliopita wa vuli, ambapo mamia ya watoto waliugua mara moja au inavyoonekana kwenye shule za chekechea za kawaida wakati wa milipuko ya Virusi vya Noro. Utazingatia maarifa haya?
Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Pettersen: Manispaa ya Trondheim inategemea tathmini na miongozo kutoka Kurugenzi ya Afya ya Norway na mashirika mengine ya umma na tathmini ambazo zimetolewa na tafiti za kimataifa na mapendekezo ya kimataifa yanayopatikana. Nchini Norway, watoto wachache wamethibitishwa kuambukizwa, pia ni kwa sababu watoto wachache wamepimwa. Watoto katika kila umri wanaweza kuambukizwa na inawezekana wakawa na dalili na kuweza kuambukiza wengine. Njia tunayotumia inahusiana na tathmini za umma, za kitaifa ambazo zimetengenezwa na pia tunaamini kuwa ni tathmini nzuri.

- Ni vitu gani muhimu zaidi ambazo sisi kama wazazi au walezi tunaweza kufanya kabla ya shule za chekechea kufunguliwa tena?
Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Pettersen: Ninadhani jambo la muhimu zaidi kufanya ni kushiriki msisimko huu na wengine na kuongea vyema kuhusu kile kitakachotendeka. Rudia, kwa kiasi, umuhimu wa kunawa mikono. Ni muhimu pia wazazi kuwa wajasiri na kutuamini wakijua kwamba tutjitahidi kudumisha hatari ya chini inayohusishwa na shule za chekechea.

Kumbuka! Wazazi na walezi pia wanahimizwa kuwasiliana na shule zao za chekechea

wakiwa na maswali yoyote.